# HALMASHAURI YA WILAYA YA MSALALA

## MUHTASARI WA KIKAO CHA KAWAIDA CHA KAMATI YA FEDHA, UONGOZI NA MIPANGO ROBO YA KWANZA KILICHOFANYIKA KATIKA UKUMBI WA HALMASHAURI YA WILAYA YA MSALALA TAREHE 25.10.2021

**WAJUMBE WALIOHUDHURIA:**

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| 1. | Mhe. Mibako Mabubu | - | Diwani Kata ya Chela | - | Mwenyekiti |
| 2. | Mhe Frola Sagasaga | - | Diwani Kata ya Mwalugulu | - | Mjumbe |
| 3. | Mhe. Ibrahim S.Masanja | - | Diwani Kata ya Mwakata | - | " |
| 4. | Mhe. Joseph B. Manyala | - | Diwani Kata yaSegese | - | " |
| 5. | Mhe. Mwashi Mgeja | - | Diwani Viti Maalum | - | " |
| 6. | Mhe. Alexander Mihayo | - | Diwani Kata ya Busangi | - | " |
| 7. | Mhe. Samwel Magema | - | Diwani Kata yaKashishi | - | " |
| 8. | Mhe. Hamisa K. Miano | - | Diwani Viti Maalum | - | " |
| 9. | Mhe. Idd Kassim Idd (MB) | - | Mbunge Jimbo La Msalala | - | " |
| 10. | Dr.. Ntanwa Kilagwile | - | Kaimu Mkurugenzi Mtendaji (W) | - | Katibu |

**WATAALAM WALIOHUDHURIA**

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 1. | Ndg | Mary J. Nziku | - | Afisa Utumishi (W) |
| 2. | " | Swalehe J. Iyulu | - | Afisa Nyuki (W) |
| 3. | " | Matias Gungumka | - | Afisa Mazingira (W) |
| 4. | " | Jane Kihahi | - | Kaimu Mganga Mkuu (W) |
| 5. | " | George I. Magembe | - | Mratibu wa CSR |
| 6. | " | Humphrey Peter | - | Afisa Misitu (W) |
| 7. | " | Ignace Lufulila | - | Afisa Ustawi wa Jamii (W) |
| 8. | " | Seleka S. Ntobi | - | Afisa Elimu Sekondari (W) |
| 9. | " | Marco E. Badehe | - | Kaimu Katibu TSC (W) |
| 10. | " | Gaspar S. Kiyabo | - | Mratibu Dawati la uwezeshaji wananchi kiuchumi (W) |
| 11. | " | Martine J.Lutego | - | Kaimu Afisa Ugavi & Manunuzi (W) |
| 12. | " | Leonard M. Mabula | - | Kaimu Mwanasheria (W) |
| 13. | " | Giringai O.Mahemba | - | Mratibu wa CHF (W) |
| 14. | " | Victoria F. Lusana | - | Afisa Tarafa Msalala |
| 15. | " | Goodluck G. Temba | - | Afisa Ushirika (W) |
| 16. | " | Raphael L. Ikombe | - | Mthibiti Ubora wa Shule (W) |
| 17. | " | Rehema Mahinyila | - | Kaimu Meneja wa CHF (W) |
| 18. | " | Giringai O. Mahemba | - | Kaimu Msajili wa Mashirika |
| 19. | " | Karim O. Balama | - | Kaimu Mkaguzi wa ndani (W) |
| 20. | " | Julius Tungura | - | Mratibu wa TASAF III |
| 21. | Eng. | Ramadhan Seleman | - | Kaimu Mhandisi wa Ujenzi (W) |

SEKRETARIETI

1. Ndg. Ibrahim A. Msumai - Afisa Utumishi
2. " Tatu S. Mshamu - Katibu Muhtasi
3. " Paschal Ngeleja - Mhasibu

- "

**MUHT.NA.FUM/72/2021/22 KUFUNGUA KIKAO**

Mwenyekiti alifungua kikao mnamo saa 5:40 asubuhi na kuwakaribisha wajumbe wote kushiriiki kikamilifu katika kikao hicho.

**MUHT.NA.FUM/73/2021/22 KURIDHIA AJENDA ZA KIKAO**

Wajumbe waliridhia ajenda 13 ambazo ni kama ifuatavyo:

1. KufunguaKikao
2. Kuridhia ajenda za kikao
3. Kusoma na kuthibitisha Muhtasari wa kikao cha kawaida cha tarehe 23.09.2021
4. Yatokanayo na Muhtasari wa kikao cha kawaida cha tarehe 23.09.2021
5. Taarifa ya Mapato na Matumizi kwa kipindi cha kuishia 30 Septemba, 2021
6. Taarifa ya Mkaguzi wa ndani robo ya kwanza (Julai – Septemba, 2021)
7. Taarifa ya watumishi kwa mwezi Septemba,2021
8. Taarifa ya mapokezi ya fedha za Ustawi wa maendeleo ya Taifa na Mapambano dhidi ya UVIKO – 191.
9. Taarifa ya tatmini ya ujenzi wa Hospitali ya wilaya ya Msalala
10. Taarifa ya Utekelezaji wa shughuli za Halmashauri ya wilaya ya Msalala kipindi cha robo ya kwanza Julai - Septemba, 2020/21
    - Idara ya Utawala na Utumishi
    - Idara ya Mipango Takwimu na Ufuatiliaji
    - Sheria
    - TEHAMA
    - Bodi ya Zabuni
11. Kusudio la kuandaa mchoro wa mipango miji na kupima viwanja kwa ajili ya matumizi ya uwekezaji wa viwanda vidogo vidogo
12. Taarifa ya ziara ya Kamati ya Fedha, Uongozi na Mipango robo ya kwanza 2021.

13. Kufunga Kikao.

**MUHT.NA.FUM/74/2021/22 KUSOMA NA KUTHIBITISHA MUHTASARI WA KIKAO CHA KAMATI YA FEDHA, UONGOZI NA MIPANGO CHA TAREHE 23.09.2021**

Wajumbe walipitia Muhtasari tajwa hapo juu na kuridhia kuwa ni sahihi kwa kumbukumbu za Halmashauri

**MUHT.NA.FUM/75/2021/22 YATOKANAYO NA MUHTASARI WA KIKAO CHA KAMATI YA FEDHA, UONGOZI NA MIPANGO CHA TAREHE 23.09.2021**

- **Ufuatiliaji wa Majengo yaliyokuwa Ofisi ya Makao Makuu ya Halmashauri ya Wilaya ya Msalala**

Kufuatia majengo ya Msalala yaliyoko Igomelo kuchukuliwa na Manispaa ya Kahama wajumbe waliazimia kuwa Mwenyekiti awasiliane na Mbunge ili waende kufuatilia; katika utekelezaji ilielezwa kuwa Mbunge wa jimbo la Msalala Mhe.Idd Kassim Idd pamoja na Makamu Mwenyekiti wa Halmashauri Mhe.Flora Sagasaga walikwenda na wakakutana na Waziri wa TAMISEMI pamoja na Mwanasheria wa Wizara ambapo Waziri alimwagiza Katibu Mkuu kutangaza katika gazeti la serikali ili ijulikane kuwa ni mali halali ya Halmashauri ya wilaya ya Msalala na ufuatiliaji bado unaendelea.

Mhe.Joseph Manyala alishauri wachaguliwe watu ili waende Dodoma kufuatilia majengo hayo ili Halmashauri ya wilaya ya Msalala iweze kuwa na hati miliki ya majengo hayo maana ajenda hiyo imekuwa ni ya muda mrefu.

Mhe. Idd Kassim Idd alisema kuwa suala hilo linafuatiliwa sana na limefika mwisho kwani Mwanasheria wa TAMISEMI alishafanya kazi na amebaki Waziri tu kulihitimisha na akashauri Mwanasheria wa Halmashauri ya wilaya ya Msalala hatiya mashitaka (demand note) Iii waliopo kwenye majengo hayo waondoke na suala la kuunda timu iende Dodoma ni kupoteza muda na fedha za serikali na kama italazimu kwenda; yeye (Mbunge) yuko tayari kugharimia safari hiyo.

Mhe. Flora Sagasaga alishauri kuwa vi vyema tu timu nyingine ingeenda Dodoma kufuatilia sualahilo kuliko kuendelea kusubiri tangazola serikali (GN) ili halmashauri isiendelee kupoteza mapato.

Kaimu Mkurugenzi Mtendaji (W) alieleza kuwa suala la majengo lisichanganywe na suala la fedha za ushuru wa huduma ambazo halmashauri ya Msalala inaidai Halmashauri ya wilaya ya Nyang'hwale maana Halmashauri ya wilaya ya Msalala haina mgogoro na mtu yoyote kuhusu majengo kinachotakiwa ni Mwanasheria wa Halmashauri afanye ufuatiliaji wa hati miliki ya majengo hayo badala ya kusubiri Waziri aje na hata timu ikienda kwa wakati huo Waziri atakuwa bungeni hivyo kuonana naye ingekuwa ni vigumu.Wajumbe walikubaliana kuwa ufuatiliaji uendelee.

- **Ufuatiliaji wa fedha za ushuru wa huduma ambazo Halmashauri ya wilaya ya Msalala inaidai Halmashauri ya wilaya ya Nyang'hwale**

Kutokana na fedha za ushuru wa huduma zinazotolewa na mgodi wa Bulyanhulu kuchukukuliwa na Halmashauri ya Nyang'hwale wajumbe waliazimia kuwa Mhe. Mbunge wa Jimbo la Msalala na Mwenyekiti wa Halmashauri waende Dodoma kufuatilia suala hilo; katika utekelezaji ilielezwa kuwa Mh.Mbunge na Mh.Mwenyekiti walienda Dodoma na kukutana na Waziri na ufuatiliaji bado unaendelea.

Mhe. Idd K.Idd alionana na uongozi wa kampuni ya Twiga Barrick Bulyanhulu na wao wakasema hawana tatizo ila kinachosubiriwa ni Halmashauri za Msalala na Nyang'hwale wakutane na waunde kamati haraka ili maridhiano yafikiwe. Kamati hiyo itaongelea masuala mengi yakiwemo ya 'Local Content', CSR, Madeni ya nyuma ya Barrick pamojana fedha za ushuru wa huduma kati ya halmashauri hizo mbili kutoka katika mgodi wa Barrick. Vie vile Mhe. Idd Kassim Idd aliomba yawepo mawasiliano ya karibu baina ya Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji na ofisi ya Mbunge wa jimbo la Msalala ili waweze kujadili suala la fedha hizo

Mratibu wa fedha za CSR alieleza kuwa Halmashauri iliwasiliana na mgodi wa Barrick Bulyanhulu na wakakubaliana kufanya kikao cha pamoja cha wataalam (Technical Committee) mnamo tarehe 26 Oktoba, 2021 katika kata ya Bugarama.

Wajumbe walikubaliana kuwa aende mtaalam mmpja tu katika kikao hicho ili akasikilize tu kinachojadiliwa ili baadaye kije kiitishwe kikao rasmi cha kamati ya CSR na kiitishwe haraka ili kuokoa fedha hizo toka mgodini.

- **Suala la ubadilishaji wa sheria ndogo**

Kufuatia Halmashauri ya Msalala kuwa na ushuru wa mpunga wa sh 2,000 kwa gunia na Halmashauri jirani za Nyang'hwale, Mbogwe, Shinyanga vijijini na Nzega kutoza sh.1,000 kwa gunia, wajumbe wa Kamati ya Fedha, Uongozi na Mipango baada ya kukasimiwa na Baraza la Madiwani walimwagiza Mwanasheria (W) afanye mabadiliko ya sheria ndogo ili Halmashauri ya wilaya ya Msalala ianze kutoza sh.1,000 kwa gunia.Katika utekelezaji ilielezwa kuwa Tangazo kwa ajili ya sheria ndogo kwa muda wa siku 21 kuanzia tarehe 25.09.2021 hadi tarehe 16.10.2021 lilitolewa. Kamati za Maendeleo za Kata zilitakiwa kukaa na kuwasilisha mihtasari hiyo tarehe 26.10.2021 bila kukosa kwa ajili ya hatua inayofuata. Wajumbe walikuballiana na maelezo hayo

**MUHT.NA.FUM/76/2021/22 TAARIFA YA MAPATO NA MATUMIZI KWA KIPINDI CHA KUISHIA TAREHE 30 SEPTEMBA, 2021**

Mweka Hazina (W) kwa niaba ya Mkurugenzi Mtendaji (W) aliwasilisha taarifa ya mapato na matumizi kwa kipindi kinachoishia tarehe 30 Septemba, 2021 kwa muhtasari kama majedwali yanavyoonekana hapa chini:-

**A: MCHANGANUO WA MAPATO**

| MAELEZO | BAJETI 2021/2022 | JUMLA YA MAPATO JULAI –AUGUST 2021 | MAPATO SEPTEMBA 2021 | JUMLA YA MAPATO JULAI SEPTEMBA 2021 | % |
|---|---|---|---|---|---|
| **Mapato ya ndani** | 4,120,000,000 | 1,048,746,575 | 181,431,394.24 | 1,230,177,969 | **30** |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| **CSR** | 2,530,000,000 | 0 | 0 | 0 | **0** |
| **Mapato lindwa** | 531,061,000 | 17,002,650.46 | *12,325,026* | *29,327,676.46* | **6** |
| **Mishahara** | 17,531,688,902 | 2,760,518,100 | 1,400,306,800 | 4,160,824,900 | **24** |
| **matumizi mengineyo (OC)** | 983,373,020 | 163,841,583.32 | 24,711,583 | 188,553,166 | **23** |
| **Ruzuku ya maendeleo** | 9,216,026,296 | 862,785,961.68 | 141,869,826 | 1,004,655,788 | **11** |
| **JUMLA** | **34,912,119,198** | **4,852,894,870** | **1,770,644,629.24** | **6,613,539,499** | **19** |

**B: MCHANGANUO WA MATUMIZI**

| **MAELEZO** | **BAJETI 2020/2021** | **JUMLA YA MATUMIZI JULAI-AGOSTI 2021** | **MATUMIZI SEPTEMBA 2021** | **JUMLA YA MATUMIZI JULAI- SEPTEMBA – 2021** | **%** |
|---|---|---|---|---|---|
| Matumizi ya kawaida (Mapato ya ndani) | **2,477,000,000** | 393,549,323 | 304,060,956 | 697,610,279 | **28** |
| Miradi ya Maendeleo (Mapato ya ndani) | **1,642,969,980** | 30,000,000 | 206,000,000 | 236,000,000 | **14** |
| CSR | **2,530,000,000** | 0 | 0 | 0 | **0** |
| Mapato Lindwa | **531,061,000** | 16,283,000 | 16,715,838 | 32,998,838 | **6** |
| Mishahara | **17,531,688,902** | 2,760,518,100 | 1,403,006,800 | 4,163,524,900 | **24** |
| Matumizi mengineyo (OC) | **983,373,020** | 170,951,000 | 11,570,000 | 182,521,000 | **19** |
| Miradi ya mandeleo (Ruzuku) | **9,216,026,296** | 95,246,856 | 285,376,703 | 380,623,559 | **4** |
| JUMLA | **34,912,119,198** | **3,466,548,279** | **2,226,730,297** | **5,693,278,576** | **16** |

Wajumbe walipokea taarifa hiyo na kujadili kama ifuatavyo:

Mhe. Idd Kassim Idd alitaka kujua fedha kiasi cha Tsh 100,000,000 za ufungaji wa mfumo wa GoTHOMIS zimetumika kufunga vituo vingapi na kuhusu faida ya uuzaji wa madawa katika vituo vya kutolea huduma za afya halmashauri imepata faida kiasi gani.

Kuhusu vyanzo vya mapato alisema Msalala ina vyanzo vingi vya mapato hasa migodi ya dhahabu kupitia ushauru wa mawe. Aidha alisema ushuru wa mpunga kuanzia mwezi Oktoba, 2021 umeshuka kutoka Tsh. 2,000 hadi Tsh 1,000 kwa gunia lakini bado bajaj na magari mengi yanapita tu bila kutozwa ushuru.

Kuhusu suala la ujenzi wa uzio katika mnada wa Bulige ambao umepelekewa kiasi cha milioni 80 akataka kujua faida itakayopatikana kwa kujenga uzio huo kama kutakuwa na tofauti kimapato na minada mingine kama Masabi ambayo haina uzio.Aidha Mhe. Idd Kassim Idd alisema soko la dhahabu lililoko Kahama Manispaa limeanza kuvuja akashauri Halmashauri ingeshirikiana na Ofisi ya Madini ili kupata takwimu halisi ya uuzwaji wa dhahabu na kukusanya ushuru kwa urahisi bila kupoteza hata senti.

Mweka Hazina (W) alisema ni kweli Msalala ina vyanzo vingi vya mapato na mkakati uliopo ni kuibua miradi mingi ya kimkakati badala ya kutegemea ushuru wa huduma kutoka katika mgodi wa Bulyanhulu pekee. Aidha alieleza kuwa mpaka wakati huo vituo vya Afya vinne (04) vya Lunguya, Bugarama, Chela na Ngaya vimefungiwa mfumo wa GoTHOMIS ambako mapato yamepamda tofauti na vituo ambavyo havina mfumo huo.

Mweka Hazina (W) aliendelea kueleza kuwa katika kudhibiti mapato yasivuje, Halmashauri ya Msalala imewezakununua pikipiki 18 kwa ajili ya Maafisa Watendaji wa kata ambazo zimegharimu kiasi cha Tsh 68,412.00 na zinatarajia kukabidhiwa kwa wahusika katikakikao cha Baraza la Madiwani la robo ya pili (Januari, 2022). Vile vile Halmashauri ilitarajia kupokea gari mbili mpya na mbili kutoka gereji wakati wowote kuanzia Oktoba, 2021 ambazo baadhi yake zitatumika katika ukusanyaji wa mapato.

Aidha alieleza kuwa makusanyo ya ushuru wa mawe katika mgodi mpya wa Busulwangili ulikuwa ni Tsh 2,000,000 kila sikuna soko la dhahabu la Kahama halmashauri inakusanya Tsh.6,000,000 kwa wiki na hiyo ni baada ya kufungwa kwa mfumo unaotambua dhahabu ilikotoka mfumo ambao umefungwana Wizara ya madini.

**MUHT.NA.FUM/77/2021/22 KUPITIA NA KUJADILI TAARIFA YA MKAGUZI WA NDANI ROBO YA KWANZA, 2021/2022**

Kaimu Mkaguzi wa ndani (W) aliwasilisha taarifa ya ukaguzi wa ndani robo ya kwanza ikiwa na hoja za nyuma na za robo husika.Hoja za robo hiyo zilikuwa ni kama ifuatavyo:

- ✓ Ukosefu wa Sheria ndogo za ukusanyaji mapato kwenye vyanzo mbalimbali
- ✓ Ukiukaji wa Kanuni za ununuzi katika utoaji wa zabuni kiasi cha Tsh.25,578,000
- ✓ Malipo yanayoungwa mkono na fomu za hati msako hazina tarehe kiasi cha Tsh.57,050,000
- ✓ Gharama za vifaa vya ujenzi kuwa juu zaidi ya bei halisi Tsh.6,190,000
- ✓ Malipo yaliyolipwa zaidi kwa Wazabuni kiasi cha Tsh.5,871,600
- ✓ Vifaa vya ujenzi vimewasilishwa, vimepokelewa lakini havionekani stoo Tsh.26,933,000
- ✓ Kasi ndogo katika utekelezaji wa ujenzi wa shule ya sekondari ya wasichana ya Bulyanhulu Tsh.150,000,000
- ✓ Madeni ya muda mrefu ambayo halmashauriinadai Tsh.5,217,141,591
- ✓ Madeni ambayo Halmashauri inadaiwa Tsh.1,347,137,259
- ✓ Kiasi cha fedha kilichokusanywa kama malipo ya papo kwa papo kilichowasilishwa kwenye taarifa ya fedha kimepunguzwa kwa Tsh.38,264,180
- ✓ Kukosa uhalisia wa mkopo wamuda mfupi katikabenki ya TIB kiasi cha Tsh.1,399,818,868
- ✓ Mapato pungufu yaliyoripotiwa katika taarifa ya mtiririko wa fedha Tsh. 1,427,907,790
- ✓ Kiasi pungufu cha PPE kimeripotiwa katika taarifa ya fedha Tsh.3,644,644,028.03

- ✓ Kiasi pungufu cha ada ya shule ya sekondari kimeripotiwa katika taarifa ya fedha Tsh 1,705,000
- ✓ Kiasi kikubwa zaidi cha mtiririko wa fedha kwashughuli za uwekezaji kimeripotiwa kwenye taarifa ya fedha Tsh 356,267,881
- ✓ Kuchelewa kuanza kwa ulipaji wa mikopo kwa vikundi vya Wanawake, Vijana na watu wenye ulemavu Tsh 152,000,000
- ✓ Mikopo iliyomaliza muda wake wa marejesho ya vikundi vya Wanawake, Vijana na Watu wenye ulemavu
- ✓ Fedha za mfuko wa TASAF hazikutolewa kiasi cha Tsh.290,739,965.25

Baada ya hapo wajumbe walipokea taarifa hiyo na kujadili kama ifuatavyo:

Mhe.Idd Kassim Idd alisema gharama za manunuzi zilikuwa ziko juu na akatoa mfano ujenzi wa shule ya Sekondari ya Busulwangili, zahanati ya Matinje, Mwanase na kwinginekohivyomiradi mingi thamanui ya fedha haionekani.Vile vile akasisitiza suala la kutembelea vyanzo vya mapato akitolea mfano katika kituo cha Afya cha Lunguya kwamba kilikuwa kikikusanya Tsh 50,000 kwa siku fedha za papo kwa papo kabla hawajatembelewa;lakini Mhe. Mbunge alifanya ziara katika kituo hicho na sasa makusanyo yamepanda na wanakusanya Tsh 400,000 kwa siku na walitarajia kukusanya Tsh 12,000,000 kwa mwezi Oktoba, 2021/

Wajumbe walikubaliana kuwa wahusika walionunua vifaa halafu vifaa vikawa havipo waitwe mbeleya kamati ili waeleze vifaa hivyo vilienda wapi.Vile vile Kamati ilimwagiza Mkaguzi wa ndani kufanya ukaguzi wa fedha za CSR kuanzia mwaka 2017 hadi 2021.

**MUHT.NA.FUM/78/2021/22 TAARIFA YA WATUMISHI KWA MWEZI SEPTEMBA, 2021**

Kaimu Afisa Utumishi (W) aliwasisha taarifa ya watumishi akieleza kuwa Halmashauri ya Wilaya ya Msalala ilikuwa na watumishi ni 1,815 ambapo jumla ya watumishi 52 wako masomoni hadi sasa. Katika mwezi Septemba kuna mtumishi mmoja amehama ambapo watumishi watatu wamehamia kutoka halmashauri mbalimbali, hakuna mtumishi aliyeondolewa na aliyerudishwa kwenye mfumo wa malipo ya mishahara (payroll)

Kwa mwezi Septemba, 2021 hakuna mtumishi aliyepandishwa cheo hii ni kutokana na kutopata ikama/Idhini ya kuwapandisha vyeo watumishi kutoka mamlaka husika. Wajumbe waliipokea taarifa hiyo na kuridhia.

**MUHT.NA.FUM/79/2021/22 TAARIFA YA MAPOKEZI YA FEDHA ZA USTAWI WA MAENDELEO YA TAIFA NA MAPAMBANO DHIDI YA UVIKO-19**

Mweka Hazina (W) aliwasilisha taarifa akieleza kuwa Serikali ya awamu ya (6) Sita chini ya Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika kutekeleza azima yake ya kuwaletea wananchi Maendeleo imeipatia Halmashauri ya Msalala kiasi cha Tsh.**2,410,000,000.00** kwa ajili ya kutekeleza Miradi katika sekta mbalimbali kama Sekta ya Elimu Msingi shule shikizi 10 vyumba 21 jumla ya Tsh **420,000,000**, Sekta ya Elimu Sekondari shule 20 vyumba 69 jumla ya Tsh **1,380,000,000** na Sekta ya Afya miundo mbinu mitatu yenye jumla ya Tsh **610,000,000**

Aidha kupitia Idara ya Afya, Halmashauri itapokea Magari 2,Gari la kwanza ni kwa ajili ya kubebea wagonjwa (Ambulance) na la pili ni kwa ajili ya shughuli za usimamizi na ufuatiliaji wa shughuli za Afya.

Wajumbe waliipokea taarifa hiyo na kujadili kama ifuatavyo:

Mhe.Joseph Manyala alitaka kujua gharama ya usombaji wa vifaa maana alipata taarifa kuwa vitaletwa na Mzabuni mmoja na kuweka makao makuu ya Hlmashauri ya wilaya ya Msalala.

Kaimu Afisa Mipango (W) alieleza kuwa ni kweli vifaa vyote yaani saruji, nondo,mbao na mabati vitanunuliwa kwa pamoja ili kupunguza bei ya vifaa vya ujenzi kama vitanunuliwa tofauti tofaut bei inaweza kupishana.

Mhe. Flora Sagasaga alitoa ushauri kuwa ni bora wasimamizi wa kila kata wajipange ili lawama isiwepona akataka kujua kuhusu nani atawajibika kutoa hela ya nauli ya kusafirisha vifaa kwenda kila kata

Mhe. Ibrahim S. Masanja alikuwa na wasiwasi juu ya bei ya vifaa na kusema ni kubwa sana mfano bei ya saruji kuna sehemu zingine bei ilikuwa inauzwa mpaka Tsh 17,000 kwa kila mfuko tofauti na bei ya Mzabuni wa jumla ya Tsh 22,000 bila gharama ya usafirishaji.

Mhe.Joseph Manyala alisemani vema kila kata ingenunua vifaa kwenye kata zao maana kwa kata ya Segese saruji ilikuwa inauzwa kwa Tsh 18,000 kwa kila mfuko na hakuina gharama ya usafirishaji.

Kaimu Afisa Mipango alieleza kuwa hayo ni maagizo toka juu na hiyo inasaidia kuondoa lawama kama vifaa vitachelewa hakutakuwa na kulaumiwa kwa kuchelewa huko. Aidha alieleza kuwa saruji ilitarajiwa kuwa inashushwa katika vituo vine vya Isaka, Ntobo, Segese na Bugarama na Halmashauri itahusika kusafirisha saruji hiyo hadi mahali panapohusika. Baada ya majadiliano hayo wajumbe waliipokea taarifa hiyo na kuridhia.

**MUHT.NA.FUM/80/2021/22 TAARIFA YA TATMINI YA UJENZI WA HOSPITALI YA WILAYA YA MSALALA**

Mweka Hazina (W) aliwasilisha taarifa ya tathmini akieleza kuwa_katika Mwaka wa Fedha 2019/2020 Halmashauri ilipokea jumla ya shilingi. 654,677,780.00 kwa ajili ya kuanza ujenzi wa Hospitali ya Wilaya ya Msalala awamu ya kwanza. Fedha hizo zilipokelewa katika akaunti ya Halmashauri tarehe 30.04.2020.Hadi kufikia Juni, 30 2020 kiasi cha fedha zilizokuwa zimetumika ni Sh. 177,083,963.00 na kiasi cha Tsh. 477,593,817.19 zilirejeshwa mfuko mkuu wa Serikali (Hazina).

Katika Mpango na Bajeti mwaka wa fedha 2020/21, Halmashauri ilipokea Jumla ya Sh. 1,000,000,000.00 kwa ajili ya kuendeleza ujenzi wa mradi huu kwa awamu ya pili.
Ujenzi uliendelea Kama kawaida na mpaka wakati huo jumla ya **Tsh 328,350,390.00** zilikuwa zinahitajika kwa ajili ya ukamilishaji wa ujenzi huo kama ifuatavyo:

| S/Na. | Aina ya Jengo | Kiasi kinachohitajika |
|---|---|---|
| 1. | wagonjwa wa nje (OPD) | 62,618,500.00 |
| 2. | Maabara (Laboratory) | 50,881,000.00 |
| 3. | Wodi ya mama na mtoto (maternity | 115,975,000.00 |

| | | |
|---|---|---|
| 4. | Kichomea taka (Incenerator) | 6,773,000.00 |
| 5. | Kufulia nguo (Laundry) | 92,102,890.00 |
| | **JUMLA** | **328,350,390** |

Wajumbe walijadili kama ifuatavyo:

Mhe. Ibrahim S. Masanja alieleza kuwa taarifa iliyotolewa na hali halisi ya ujenzi wa hospitali hiyohaviwiani hata kidogo.

Mhe. Alexander Mihayo alishangazwa na matumizi ya vifaa vya ujenzi kama vile mbao na mabati kukatwa katwa ovyo ovyo tu na kutupwa na akahoji iweje mabati yakatwe katwe wakati viwanda hutengeneza mabati kwa futi kulingana mahitaji ya mtumiaji

Mhe. Flora Sagasaga alishangaa kuona ujenzi wa hospitali hiyo Wilaya ya Msalala kutokamilika wakati Mhandisi wa Ujenzi (W) alikuwa ameieleza Kamati ya Siasa ya Mkoa kuwa fedha iliyokuwa imetolewa ilikuwa inatosha kukamilisha ujenzi huo na kubakia na ndiyo sababu likaanzishwa jengo jingine la kufulia ambapo ilielezwa kuwa lingeishia mahali na kukamilishwa kwa fedha za mapato ya ndani. Akataka kujua kwanini lilianzishwa jengo na likasababisha majengo ya hospitali kutokukamilika; akashauri ni vyema kingefanyika kikao maalum cha kamati ya Fedha, Uongozi na Mipango ilikuweza kujadili na kuchambua kwa kina hatua moja baada ya nyingine.

Wajumbe walikubaliana kuwa kifanyike kikao maalum cha kamati kiweze kujadili taarifa hiyo ya ujenzi wa hospitali ya wilaya kabla ya kikao cha Baraza la Madiwani.

**MUHT.NA.FUM/81/2021/22 KUPITIA TAARIFA ZA UTEKELEZAJI ROBO YA KWANZA JULAI – SEPTEMBA, 2021**

- **Mipango,Takwimu & Ufuatiliaji**

Kaimu Afisa Mipango (W) alieleza kuwa, Idara ilijipangia na kufanikiwa kutekeleza shughuli mbalimbali kama ilivyoainishwa hapo chini;

- ✓ Usimamizi na ufuatiliaji wa miradi ya maendeleo
- ✓ Watumishi wa Idara ya Mipango, Takwimu na Ufuatiliaji waliweza kutimiza majukumu yao
- ✓ Kikao cha Kamati ya Lishe ya Halmashauri kilifanyika

Changamoto na mikakati ya kukabiliana na changamoto hizo iliwasilishwa na wajumbe waliipokea taarifa hiyo na kuridhia.

- ➢ **Utumishi & Utawala**

Kaimu Afisa Utumishi (W) alielezakuwa katika kipindi cha mwezi Julai hadi mwezi Septemba 2021, Idara ya Utawala na Utumishi, ilipanga na kufanikiwa kutekeleza shughuli saba (7) ambazo ni;

- ✓ Kuwawezesha usaidizi wa chakula kwa watumishi 3 wa Halmashauri waliojitokeza, wanaoishi na VVU
- ✓ Kuwezesha Halmashauri kulipa ankara mbalimbali (maji, umeme, simu, fax, posta, mafuta, intaneti, ulinzi na gharama za uendeshaji Ofisi)
- ✓ Kumuwezesha Mkurugenzi Mtendaji (W) kukarimu wageni waliomtembelea ofisini
- ✓ Kuwezesha vikao vya Halmashauri vya kisheria kufanyika
- ✓ Kumwezesha Mwenyekiti wa Halmashauri kutimiza majukumu yake

Changamoto na Mikakati ya kukabiliana na changamoto zilizojitokeza iliwasilishwa na wajumbe waliipokea taarifa hiyo na kuridhia.

- ➢ **Sheria**

Kaimu Mwanasheria (W) Majukumu ya kitengo cha Sheria ni pamoja na kutoa ushauri wa kisheria kwa Halmashauri, Kuiwakilisha Halmashauri Mahakamani, Kuandaa Sheria Ndogo za Halmashauri pamoja na marekebisho yake pindi kuna uhitaji wa kufanya hivyo. Kuandaa na kusimamia Mikataba mbali mbali ya Halmashauri, Kusimamia utekelezwaji wa Sheria Ndogo za Halmashauri na Sheria zingine za Nchi kwa jumla.

Katika kipindi cha robo hiyo ya kwanza (Julai- Septemba) ya mwaka wa Fedha 2021/2022. Kitengo cha Sheria katika mpango wake wa kazi kilipanga na kufanikiwa kutekeleza shughuli mbili kama ifuatavyo:

- ✓ Kuiwakilisha Halmashauri katika kesi mbalimbali zilizopo katika Mahakama Kuu Registry ya Shinyanga, Mahakama ya Wilaya ya Kahama, Baraza la Ardhi na Nyumba la Wilaya Kahama na Tume ya Usuluhishi wa Migogoro ya Kazi iliyopo Kahama jumla ya kesi nne (04)
- ✓ Kuandaa Sheria Ndogo mpya nne na kufanya marekebisho ya Sheria Ndogo za Ada na Ushuru za Halmashauri. hapo juu.

Mwenendo wa kesi zilizokuwepo katika robo hiyo, changamoto na mikakati ya kukabiliana na changamoto hizo ziliwasilshwa na Wajumbe waliipokea taarifa hiyo na kuridhia

➢ **Ugavi na Manunuzi**

Kaimu Afisa Ugavi na Manunuzi (W) alieleza kuwa kwa mujibu wa Sheria Na.7 ya mwaka 2011 na Kanuni zake za mwaka 2013 Kifungu cha 60(4) na Kanuni ya 231 (3). Aidha kwa mujibu wa Sheria ya fedha Kifungu Na. 290 Tamko la Serikali Na. 330 la mwaka 2014 na kanuni Na 17 (b) zinamtaka Afisa Masuuli kuwasilisha taarifa na michakato yote ya manunuzi kwenye Kamati ya fedha, Mipango na Uongozi.

Halmashauri imeweza kufanya manunuzi kwa kutumia mfumo mpya wa manunuzi kwa njia ya ki–elektroniki (TANePS), manunuzi madogo ya dharura" (Micro Value Procurement) na nukuu ya bei kwa kutoa LPO ( Local Purchase Order) kwenye mfumo wa MUSE kwa watoa huduma walioingia mikataba na wakala wa Ununuzi wa Huduma Serikalini (GPSA).

Katika kipindi hicho cha Julai-Septemba, 2021 Halmashauri ilifanya manunuzi ya **Tshs.133, 649,790.00** kati ya manunuzi hayo fedha zilizolipwa ni **Tshs.54, 070,000** na deni ni **Tshs. 79,579,612.00**

Changamoto na Mikakati ya kukabiliana na changamoto hizo ziliwasilishwa na Wajumbe waliipokea taarifa hiyo na kuridhia

**MUHT.NA.FUM/82/2021/22 KUSUDIO LA KUANDAA MICHORO KWA AJILI YA UJENZI WA VIWANDA VIDOGO VIDOGO**

Kaimu Afisa Ardhi na Maliasili (W) aliwasilisha taarifa ya kusudio la uandaaji wa michoro ya viwanja kwa ajili ya ujenzi wa viwanda vidogo vidogo ambapo alieleza kuwa

kipindi cha nyuma,Halmashauri ya Msalala ilikabidhiwa maeneo mbalimbali na wananchi kwa ajili ya shughuli za ujenzi na uwekezaji wa vitega uchumi pamoja na ujenzi wa majengo ya ofisi za Halmashauri. Maeneo hayo yapo sehemu mbalimbali ndani ya mipaka ya Halmashauri Kama vile Bugarama, Segese na Masabi ambapo kwa sasa yanaonekana kama yamesahaulika na kutelekezwa na Halmashauri jambo ambalo linashawishi wananchi kuanza kuyavamia taratibu na kufanya shughuli za ujenzi. Mfano ni eneo la Masabi ambapo shughuli za uchimbaji na ujenzi wa planti zinaendelea, kuna eneo (uwanja wa ndege) limeanza kuvamiwa na baadhi ya wawekezaji kutokana na kutokulipima na kulimilikisha kwa Halmashauri .

Upimaji wa viwanja utasaidia kulinda maeneo ya Halmashauri pia kukusanya mapato yatokanayo na kodi ya pango la Ardhi na kodi nyinginezo ambazo zitaingia moja kwa moja kama chanzo kingine cha mapato katika Halmashauri.

Wajumbe waliipokea taarifa hiyo mna kushaurikuwa upimaji huo ungeenda sambamba na upimaji wa viwanjavya makazi ili Wahe. Madiwani, Wataalamna Maafisa Watendajiwaweze kupatiwa viwanja walivyoahidiwa kupewa na Halmashauri ya Wilaya ya Msalala tangu muda mrefu..

**MUHT.NA.FUM/83/2021/22 TAARIFA YA ZIARA YA KAMATI YA FEDHA, UONGOZI NA MIPANGO ROBO YA KWANZA 2021.**

Mchumi aliwasilisha taarifa ya ziara ya Kamati ya Fedha, Uongozi na Mipango na kuwasilisha miradi yote iliyotembelewa ambapowajumbe waliipokea taarifa hiyo na kuridhia.

**MUHT.NA.FUM/84/2021/22 KUFUNGA KIKAO**

Mwenyekiti alifunga kikao saa 10:41 jioni, baada ya kuwashukuru wajumbe wote waliohudhuria kikao na kusisitiza maagizo yote yafanyiwe kazi.

"MUHTASARI HUU UMETHIBITISHWA"

| | | |
|---|---|---|
| ............................... | ............................... | ............................... |
| KATIBU | TAREHE | MWENYEKIT |